Kuzuia adhabu ya viboko shuleni

Majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara

Pia kwenye msururu huu:

Kupiga marufuku adhabu zote za kichapo kwa watoto:
Majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara

Kupiga marufuku adhabu zote za kichapo kwa watoto:
Maswali na majibu kwa watoto na vijana

KIMECHAPISHWA 2017 NA:

Mpango wa Kimataifa wa Kukomesha Adhabu zote za Viboko kwa Watoto (Global Initiative to End All Corporal Punishment of Children)

www.endcorporalpunishment.org

Mpango wa Kimataifa wa Kukomesha Adhabu zote za Viboko kwa Watoto umesajiliwa Uingereza na Wales kama kampuni ndogo nambari 2354395 na ya hisani nambari 328132.

Ofisi iliyosajiliwa: The Foundry, 17 Oval Way, London SE11 5RR, UK.

Shirika la Save the Children Sweden

www.raddabarnen.se; resourcecentre.savethechildren.net

Save the Children Sweden ni sehemu ya Chama cha Save the Children, Shirika la Misaada lenye mashirika 29 tofauti ya Save the children, kilichosajiliwa Uswizi na ni moja ya mashirika makubwa duniani ya Haki za Watoto. Shirika la Save the Children pia ni mmiliki wa Save the Children International (SCI), ambalo ni shirika linalotekeleza mpango wa kimataifa.

Makao Makuu ya Ofisi za Save the Children Sweden: Radda Barnen, SE-107 88 Stockholm, Landsvagen 39, Sundyberg, Sweden.

Hatua zinapochukuliwa ili kuzuia adhabu ya viboko shuleni, kuna maswali mahususi ambayo huibuka mara kwa mara. Kijitabu hiki kinatoa majibu ya baadhi ya maswali hayo na kinanuia kuweka wazi maswala makuu yanayohusika. Kinafaa kuwapa maafisa wa serikali, wataalam wa elimu na wengine wanaojihusisha kwa kupigwa marufuku, walio na ujasiri wa kushughulikia mabadiliko ya kisheria na kupiga hatua viboko kwa kutimiza haki za watoto kwa kuwalinda kutokana na aina yoyote ya vurugu katika hali zote.

Yaliyomo

Sehemu ya 1: Kanuni za Msingi

8 Watoto wana haki ya kulindwa dhidi ya adhabu ya viboko

11 Watoto wana haki ya kulindwa dhidi vurugu katika mazingira yote

12 Matatizo ya nidhamu hayafai kuonekana kama masuluhisho ya kinidhamu

Sehemu ya 2: Kupiga marufuku adhabu za viboko kwa watoto shuleni: Majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara

16 Walimu wengi hupinga kupigwa marufuku kwa adhabu ya viboko. Je, ni lazima kuwasikiza, kwani wao ndio hushughulikia utovu wa nidhamu shuleni kila siku?

18 Kwanini waalimu hupinga kupigwa marufuku kwa adhabu ya viboko?

22 Ikiwa unataka kuwafunza watoto kuhusu heshima na nidhamu, unalazimika kutumia adhabu ya viboko?

26 Bila shaka kusababisha maumivu au kifo haikubaliki, lakini ikidhibitiwa na kusimamiwa vizuri, si adhabu ya kiboko ni njia mwafaka ya sera ya kuweka nidhamu shuleni?

30 Shule nyingine za kidini husema imani zao huwahitaji watumie adhabu ya kiboko. Je, ni ubaguzi kuwazuia kuitumia?

32 Walimu wengi na wafanyakazi wengine wanafadhaika sana kwa sababu ya madarasa yaliyojaa watoto wengi na ukosefu wa rasilimali. Je, si kutoa adhabu za viboko huongezea mifadhaiko yao?

34 Tayari tunayo sera ya shule/wizara dhidi ya adhabu ya kiboko. Je, kwa nini pia ni muhimu kubadilisha sheria?

36 Sehemu ya 3: Tovuti na rasilimali zenye manufaa

Sehemu ya 1: Kanuni za msingi

Watoto wana haki ya kulindwa dhidi ya adhabu ya kichapo

Karibu kila nchi ulimwenguni imeridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto, na kwa hivyo ina jukumu la kutekeleza haki hiyo. Sheria ya 28 (2) ya Mkataba inasema kuwa njia za nidhamu za shule zinapaswa "kuendana na hadhi ya mwanadamu na kulingana na Mkataba wa sasa". Kamati ya Haki za Mtoto, ambayo inaangalia utekelezaji wa Mkataba huo, imetafsiri sheria hii kuwa ni ya kukataza adhabu ya kiboko shuleni. Mashirika ya ufuatiliaji wa mikataba mingine pia imesisitiza kwamba sheria za haki za binadamu za kimataifa na kikanda zinahitaji kukataliwa kwa adhabu ya kiboko shuleni.

Kwa hivyo kukataliwa kwa adhabu ya kiboko shuleni kunaeleweka vyema kama jukumu la haki za kibinadamu. Utafiti una nafasi nzuri katika kudhihirisha kuongezeka kwa adhabu ya kiboko, kuangalia utekelezaji wa upigaji marufuku, na kukuza njia bora, zisizo za vurugu, na shirikishi kwa nidhamu ya shule. Lakini utafiti hauhitajiki ili "kudhibitisha" kwamba adhabu ya kiboko inapaswa kupigwa marufuku shuleni: swala ni kuhusu haki za kibinadamu. Watoto wana haki ya ulinzi wa kisheria kutokana na adhabu ya kiboko 8 na Kuipiga marufuku shuleni.

Hata hivyo, kuna thibitisho kubwa la kiutafiti linaloashiria kwamba adhabu ya kiboko ina athari kali katika masomo. Katika utafiti wa hivi majuzi, matumizi ya kiboko shuleni yalihusishwa na alama duni za mtihani na athari mbaya za ustawi wa kisaikolojia na mahusiano ya watoto.[1] Vurugu shuleni – ikijumuisha adhabu ya kiboko – pia ni sababu kuu kwa nini watoto hawapendi shule na huchangia kutoroka kwao shuleni.[2]

Chini ya Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu, iliyopitishwa na viongozi wa ulimwengu mnamo Septemba 2015, nchi zimejitolea kuhamasisha juhudi za kuunda "mazingira salama ya masomo, yasiyokuwa na vurugu, husishi na yanayofaa kwa wote" (lengo la 4a) na kumaliza aina zote za vurugu dhidi ya watoto (lengo la 16.2). Kumaliza adhabu ya kiboko kwa watoto shuleni – na mipangilio yote – ni muhimu kufikia malengo haya na mengineyo ya kiafya na ya kielimu.

1. UNICEF Office of Research – Innocenti (2015), Corporal Punishment in Schools: Longitudinal Evidence from Ethiopia, India Peru and Viet Nam, Florence: UNICEF Office of Research.

2. Global Initiative (2016), Corporal punishment of children: review of research on its impact and associations, available at endcorporalpunishment.org/resources/research.

“Watoto wana haki ya kuheshimiwa kwa sababu ya hadhi yao ya kibinadamu na uadilifu wa kimwili.”

Watoto wana haki ya kulindwa kutokana na vurugu katika mipangilio yote

Jukumu la nchi kupiga marufuku adhabu ya kiboko kwa watoto hutegemea haki ya watoto ya kuheshimiwa kwa sababu ya hadhi yao ya kibinadamu na uadilifu wa kimwili, kama wanadamu. Wakati kijitabu hiki kinazungumzia mada muhimu sana ya kupiga marufuku adhabu ya kiboko shuleni na maswali maalum ambayo kinazua, serikali na wataalamu wa elimu pia wanapaswa kufahamu kwamba watoto wana haki ya kuheshimiwa kwa sababu ya hadhi yao ya kibinadamu na uadilifu wa kimwili katika mazingira yote ya maisha yao, ikijumuisha nyumbani, mipangilio ya utunzaji wa watoto, utunzaji mbadala, taasisi za adhabu na katika jeshi.

Shida za nidhamu hazipaswi kuchanganyishwa na suluhisho za nidhamu

Ni muhimu kutofautisha kati ya shida za nidhamu shuleni na njia ambazo shule zinazitatua. Kuna tabia kati ya wale ambao wanapinga dhidi ya kupiga marufuku wakiashiria tabia ya watoto kama sababu inayopelekea hitaji la adhabu ya kiboko. Lakini tabia ya watoto haiashirii majibu ya kidhuluma.

Shida za nidhamu shuleni zinatokana na mchanganyiko wa mambo mengi, ikijumuisha yale yanayohusiana na hali binafsi za mtoto, mazingira ya shule, jinsi taaluma ya ualimu inavyopatiwa mafunzo na kuungwa mkono katika nchi fulani, utoshelevu wa mtaala, na kadhalika. Nidhamu duni shuleni huwakilisha shida ya kutotambua na kutotatua ipasavyo sababu za shida zinazotambuliwa; haitokei kutokana na kutotumia adhabu ya kiboko kwa watoto.

Kushughulikia shida za kinidhamu inahitaji uingiliaji wa kitaaluma, wenye ubunifu, wa huruma, ulioungwa mkono na wenye heshima sio kuwapiga na kuwadhalilisha wanafunzi. Kuna rasilimali nyingi zinazopatikana kwa urahisi za kuanzisha na kudumisha usimamizi mzuri wa darasa huku ukiheshimu haki za kibinadamu kwa watoto (angalia Sehemu ya 3 kwa mifano iliyochaguliwa).

Sehemu ya 2: Kupiga marufuku adhabu za viboko kwa watoto shuleni:

Majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara

Walimu wengi hupinga kupigwa marufuku kwa adhabu ya kiboko. Je, ni lazima kuwasikiza, kwani wao ndio hushughulikia utovu wa nidhamu shuleni kila siku?

Serikali zinapaswa kushirikiana na walimu kuhusu changamoto zinazowakabili, hata hivyo kwa suala hili – kama mengine, ikijumuisha ukatili dhidi ya wanawake, ubaguzi wa rangi na afya ya umma – serikali zina jukumu la kuongoza, sio kufuata maoni ya umma. Msisitizo lazima uwe kwenye wajibu wa serikali wa haki za binadamu ili kuhakikisha kwamba sheria inawapa watoto, kama watu wazima, ulinzi kamili wa hadhi yao ya kibinadamu, na pia kufanya kazi pamoja na walimu na kuwaunga mkono ili kuhakikisha kwamba sheria hiyo inatekelezwa.

Ushahidi kutoka kwa utafiti pia unaonyesha wazi kuwa nidhamu chanya na isiyo na vurugu, hutoa matokeo bora darasani, huku adhabu ya kiboko ikihusishwa na matokeo mengi mabaya ikijumuisha alama za chini za IQ, misamiati midogo, uwezo duni wa utambuzi, maendeleo ya utambuzi yaliyo ya polepole, na alama duni za shule.[3]

3. Ogando Portela, M. J. & Pells, K. (2015), Corporal Punishment in Schools Longitudinal Evidence from Ethiopia, India, Peru and Viet Nam – Innocenti Discussion Paper 2015-02, Florence: UNICEF Office of Research.

Pia mara kwa mara hutolewa kama sababu ya kutohudhuria au kuacha shule.[4] Tena, ni jukumu la serikali kuongoza katika kusimamia kupitishwa kwa njia bora ya ufundishaji katika mfumo wote wa elimu, kwa kuwasaidia walimu kukuza mikakati mizuri na isiyo ya vurugu, kupitia mafunzo, msaada, rasilimali za kutosha na utawala bora wa shule, kama vile kutuma ujumbe wazi kwa njia ya kupiga marufuku kwamba adhabu ya kiboko shuleni sio halali tena.



4. Pinheiro, P. S. (2006), World Report on Violence against Children, Geneva: United Nations.

Je, kwa nini walimu hupinga upigaji marufuku wa adhabu ya kiboko?

Mbali na sababu zilizoelezwa hapo juu, kuna sababu zingine zinazoeleza kwa nini walimu wanaweza kupinga upigaji marufuku:

Tabia, mila, mazoea

Adhabu ya kiboko imekuwa ikitumika sana shuleni hapo zamani, inakubaliwa sana katika taaluma ya elimu katika nchi zingine, na inaungwa mkono na hata wakati mwingine inahimizwa na wazazi. Walimu wenyewe labda walipitia katika siku zao za shule. Na walimu wengi pia ni wazazi ambao huenda walitumia adhabu ya kiboko katika kulea watoto wao.

Lakini mambo hubadilika na jamii husonga mbele. Kutambua watoto kama wamiliki wa haki ni lazima hatua zichukuliwe za kukomesha uhalali na kitendo cha jamii kukubali unyanyasaji dhidi ya watoto, kama vile jamii ilivyosonga mbele na kukomesha unyanyasaji dhidi ya wanawake. Hili si jambo la kusukumiana lawama – kwa nyakati zilizopita, walimu wamekuwa wakiwajibika kulingana na matarajio yao katika jamii – lakini wakati umefika sasa kuwasiliana vyema na watoto.

Uhalali

Kama sheria ikiendelea kuruhusu kutandika viboko katika mashule basi itaonekana kama ni njia halali ya kukabiliana na nidhamu mashuleni. Sera, ushauri na uongozi ambao unaokuza maono mazuri ya kuonya, yatakuwa na matokeo hafifu yakishinikizwa na sheria ambayo inaruhusu utumiaji wa adhabu ya viboko. Hata ikiwa sheria ya elimu inaonekana kuwa kimya katika suala hili, watu wengi wakikubali kwa njia mmoja au nyingine kutumia viboko wakati wanapolea na

kuwaelimisha watoto walimu wanaweza kuhisi kuwa wana haki ya kutumia viboko na kusababisha maumivu na/au kumdhalilisha mwanafunzi kwa kusingizia nidhamu.

Sheria kamilifu ya kuzuia adhabu ya viboko inatoa ujumbe unaoashiria kwamba unyanyasaji wa watoto mashuleni haukubaliki tena, na hivyo inamaanisha kuanzishwa kwa mbinu zingine zenye heshima na muelekeo mzuri.

Imani

Katika shule za kidini, utumiaji wa adhabu ya viboko unaweza kuungwa mkono na kupendekezwa na baadhi ya tafsiri kutoka kwenye vitabu vya kidini. Kuna uwezekano kwamba kuna ukosefu wa uhamasisho na ufafanuzi tofauti ambao unakuza njia zisizo za unyanyasaji wa adhabu ya viboko zinazoungwa mkono na taasisi za kidini. Tazama 'Baadhi ya shule za kidini zinasema imani zao zinaamuru kutumia adhabu ya viboko. Je, ni ubaguzi wakikatazwa kutumia adhabu hiyo?' ukurasa wa 30 kwa maelezo zaidi.

Ukosefu wa maarifa

Imani ya kuwa adhabu ya viboko ni muhimu na madhubuti katika kusimamia nidhamu ya shule inaweza kusababisha kutokujua njia chanya za nidhamu, haki za watoto, maendeleo bora ya mtoto na jinsi watoto wanavyojifunza, udhaifu wa adhabu ya viboko kama njia ya kukanya na athari potofu ya adhabu hiyo kwa watoto katika maendeleo katika masomo yao, na pia kutambua tofauti kati ya adhabu na nidhamu. Walimu wanaweza wakashindwa kutambua matatizo mengi yanayowapata watoto,

ambayo yanaweza kuathiri uwezo wao wa kujifunza pamoja na tabia zao. Masuala haya yote yanatakiwa kurasimishwa na kutolewa mwanzoni mwa mafunzo ua ualimu.

Shinikizo kwa walimu

Teachers may be poorly trained, underpaid and undervalued, classes may be large, and schools may be poorly resourced. This can diminish teachers' patience and result in angry and inappropriate responses to children's behaviour, "lashing out" and difficulties in achieving good classroom management. However this cannot be a justification for teachers venting their stress on students. See 'Many teachers and other staff are under stress from having to manage overcrowded classes and due to a lack of resources. Doesn't banning corporal punishment just add to their stress?' page 32 for a fuller discussion of teacher stress.

Kuelewa hizi sababu inaweza kusaidia kushirikiana kimawazo na walimu kuhusu umuhimu wa kusitisha na kuweka viwango maalum vinavyohakikisha kwamba sheria hiyo inafuatiliwa. Lakini, viwango hivyo visitumike kama kisingizio cha kuendeleza adhabu ya viboko, hata kama ni 'hatua ya mwisho', na pia visibadilishe matakwa ya haki za binadamu ya kusitisha adhabu ya viboko.

Ni muhimu pia kutambua kwamba karibu nchi zote ambazo zimekataza adhabu za viboko majumbani, zimefanya hivyo bila kujali maoni ya umma, na baadaye maoni ya umma yameunga mkono mabadiliko. Na hii ni kweli kuhusu kusitishwa kwa adhabu hiyo mashuleni. Kuna uwezekano kwamba kuna wachache wanaoendelea kuamini adhabu ya viboko mashuleni itumike kwenye kuadabisha – mjadala ambao kwa mara nyingi unatokana na sintofahamu na upotovu wa ukweli – na kwa wengi, ifikapo siku ambapo adhabu ya viboko itakuwa sio moja ya nyenzo ya kuadhibu, na wakati ambapo walimu wanapata njia chanya za kusimamia darasa, itafika wakati ambapo kupiga watoto kwa kushindwa kufanya kazi za shule nyumbani litaonekana kama ni jambo lisiloeleweka na la upumbavu.

Je, ukitaka kuwafundisha watoto heshima na adabu, ni lazima utumie adhabu ya viboko?

Hoja hii inatokana na wazo kwamba kupiga watoto ni kwa ajili ya "faida yao". Swala hili linachanganya adabu na adhabu, na kuheshimu kwa hofu.

(i) '**Maslahi bora**' kwa mtoto. Kamati ya Haki za Mtoto inaeleza swala hili kwa kifupi katika nukuu namba 8 kuhusu "Haki ya mtoto dhidi ya adhabu ya viboko na aina nyingine za adhabu za kikatili au zenye kudhalilisha (sanaa. 19; 28, aya. 2; and 37, inter alia)" (ibara. 26):[5]

... tafsiri ya masilahi mazuri ya mtoto lazima iwe sambamba na Makubaliano yote, pamoja na jukumu la kuwalinda watoto dhidi ya kila aina ya dhuluma na umuhimu wa kushikilia maoni ya mtoto; haiwezi kutumiwa kuhalalisha desturi, kama adhabu ya viboko na aina nyingine za adhabu ya kikatili au yenye kudhalilisha, ambayo inapingana na utu wa binadamu ya mtoto na haki ya uadilifu wa mwili."

(ii) **Nidhamu dhidi ya adhabu.** Usimamizi mzuri wa darasa sio sawa na adhabu. Haitegemei mabavu, bali inakuzwa kutokana na hali ya kuheshimiana na mawasiliano bora. Adhabu ya kutandikwa viboko ni desturi mbaya inayowafundisha watoto ya kuwa watu wazima hutumia vurugu ili kutatua shida au mizozo. Katika Maoni yake ya Jumla Na. 8, Kamati ya Haki za Mtoto inaelezea kwamba ingawa adhabu ya kutandika viboko imekataliwa, nidhamu inatambuliwa kama ni jambo muhimu wakati watoto wanapokuwa (ibara. 13):

5. Available in English, French, Spanish, Arabic, Russian and Chinese at http://tbinternet.ohchr.org/_layouts/treatybodyexternal/Download.aspx?symbolno=CRC%2fC%2fGC%2f8&Lang=en

“Kwa kukataa kuhalalisha unyanyasaji na udhalilishaji wowote kama njia ya kuadhibu watoto, Kamati haikatai njia chanya za kuleta nidhamu.” Ukuaji mzuri wa watoto hutegemea wazazi na watu wazima kuwapa mwongozo na mwelekeo unaohitajika, sambamba na ubadilikaji wa uwezo wa watoto, kusaidia ukuaji wao ili wawe na maisha yenye uwajibikaji katika jamii.”

Ni kweli, kuna wakati mwingine walimu wanalazimika kutumia nguvu, kwa mfano wakikabiliana na hali ya hatari. Ikiwa hivyo, basi itikio lilingane na adhabu inayofaa, na sio kutumia nguvu nyingi, na ambayo ina lengo la kuonya na siyo la kuadhibu. Kama Kamati inavyoeleza (ibara. 15):

“Kamati inatambua kwamba kuna mazingira ambayo waalimu na watu wengine, kwa mfano; wale ambao wanafanya kazi katika taasisi za kuwasaidia watoto watukutu, wanahatari ya kukabiliana na mienendo isiyostahili ambayo inaweza kudhihirisha kutolewa kwa adhabu inayostahili. Hapa pia kuna tofauti dhahiri kati ya utumiaji wa nguvu unaohimizwa na dhamira ya kumkinga mtoto au watu wengine na utumiaji wa nguvu kwa sababu ya kuadhibu. Kanuni ya matumizi sahihi ya nguvu kidogo kwa muda mfupi ifaavyo inapaswa kutumika. Mwongozo na mafunzo ya kina pia yanahitajika, ili kupunguza uwezekano wa kutumia kizuizi na kuhakikisha kwamba njia yoyote itumikayo ni salama na mwafaka kulingana na hali iliyopo na haisababishi maumivu kama njia ya udhibiti.”

(iii) **Heshima dhidi ya hofu.** Heshima haifai kutatanishwa kuwa ni hofu. Tabia "bora" kwa kuhofia kuadhibiwa inamaanisha kwamba mtoto anaepuka adhabu na sio kuonyesha heshima. Huenda adhabu ya viboko ikaonekana kuwa mwafaka sana kwa matokeo ya haraka, lakini ni hasi kwa matokeo ya muda mfupi na muda mrefu–ikiwemo ukuaji hasi wa kihisia na kimawazo, na matokeo mabaya ya kielimu, na huchangia kuacha shule[6]– kwa hakika huwa kikwazo cha kujifunza na hudhororesha mchakato wa kufundisha na kujifunza.

Watoto hujifunza kuheshimu watu na vitu kwa dhati wakati wanafurahia thamani yao ya ndani. Walimu wanapoonyesha heshima kwa hadhi ya kibinadamu na uadilifu, watoto hujifunza kujiheshimu na kuwaheshimu wengine. Walimu wanapowaadhibu watoto kwa njia nzuri, kwa utulivu, watoto hujifunza kwamba ugomvi unaweza kusuluhishwa bila kudhoofisha heshima hii. Mitindo chanya ya kuadhibu huandaliwa ili kuhakikisha kwamba watoto wanajifunza kuwafikiria wengine na matokeo ya matendo yao. Kuna maandiko mengi ambayo yanatetea utumiaji wa mbinu sisizohusisha fujo ili kuongoza madarasa. Maandiko haya yanaweza kutumika katika nchi zote.[7]

6. Global Initiative (2016), Corporal punishment of children: review of research on its impact and associations, available at endcorporalpunishment.org/resources/research.

7. Mengi ya haya yameorodheshwa kwenye tovuti ya Mpango wa Kimataifa www.endcorporalpunishment.org; baadhi ya mifano imeainishwa kwenye Sehemu ya 3: Tovuti na rasilimali muhimu.

Kwa hakika, kusababisha majeraha au kifo ni haramu, lakini ikidhibidhiwa na kutumiwa vyema, adhabu ya viboko si njia mwafaka ya kuhakikisha uwepo wa nidhamu shuleni?

Kwa hakika, kusababisha majeraha au kifo ni haramu, lakini ikidhibidhiwa na kutumiwa vyema, adhabu ya viboko si njia mwafaka ya kuhakikisha uwepo wa nidhamu shuleni?

Maumivu ya viboko kwa mtoto ni makali kuliko yale ya kuchapwa makofi. Hata hivyo, matendo haya yote ni mwendelezo wa unyanyasaji na yanakiuka haki za mtoto za kuheshimu hadhi na uadhilifu wa kimwili. Jamii hazijaribu kutoa maana ya viwango vya nguvu vinavyokubalika wakati zinapotoa changamoto ya unyanyasaji kwa wazee, kwa mfano, wakati unyanyasaji wa aina yoyote haukubaliki. Kwa nini inakubalika kufasili viwango vya unyanyasaji vinavyokubalika kwa watoto?

Na pia sio sahihi kushauri kwamba watu wazima wana haki ya kuamua kiwango cha unyanyasaji wanachokitumia. Kusababisha maumivu ya kimwili kwa mtoto ni ukiukaji

wa haki ya watoto ya kulindwa kutokana na shambulio – na watu wazima mara nyingi hawatambui tofauti za ukubwa wa kimwili na nguvu kati yao na mtoto, na athari ambayo tofauti hii inaweza kuleta kwa walengwa na maumivu halisi ya kimwili anayohisi mtoto. Utafiti mkubwa uliofanyika ambapo wazazi waliulizwa kuhusu nguvu iliyotumika wakati wakimchapa mtoto wao uligundua kwamba wazazi wawili kati ya watano walitumia kiwango cha nguvu tofauti kuliko walivyonuia.[8] Na utafiti uliofanywa na Taasisi ya Tiba ya Akili na Chuo cha London umebainisha kwamba mabadiliko katika kazi ya ubongo wakati nguvu hutumika katika hali ya kulipiza kisasi, kwa kawaida husababisha kuongezeka kwa kiwango cha nguvu zinazotumika na kutokuwa na usahihi katika kuamua kiasi cha nguvu zinatumika.[9]

8. Kirwaun, S. & Bassett, C. (2008), Uwasilishaji kwa NSPCC: Adhabu ya viboko, Ofisi ya Utafiti wa Masoko Uingereza/Jumuiya ya Taifa ya Kuzuia Ukatili kwa Watoto .

9. Shergill, S. S. et al (2003), "Two eyes for an eye: The neuroscience of force escalation", Science, vol. 301, 11 July 2003, p. 187.

Wabunge na taasisi za serikali zimejaribu kutenganisha unyanyasaji wa mtoto na adhabu ya viboko, lakini unyanyasaji mwingi ni wa adhabu ya viboko – watu wazima kunyanyasa watoto ili waweze kuwaadhibu na kuwaongoza. Kumekuwa na kesi nyingi ambapo adhabu ya viboko inayotolewa shuleni imesababisha vifo au majeraha makubwa yasiyofutika kwa mtoto.

Kuhusiana na maendeleo ya watoto shuleni, imethibitika kwamba adhabu ya viboko inaleta athari mbaya katika maendeleo ya utambuzi na matokeo ya kielimu, na huchangia watoto kuacha shule (tazama Sehemu ya 1: Kanuni za msingi). Zaidi ya hayo, kumekuwa na mabadiliko ya uelewa wetu katika hatua ya mafunzo. Waalimu wanatambua kwamba mbali na kuwa wapokeaji wa ujuzi tu, chini ya uongozi wa waalimu, watoto wanajifunza vizuri wakijihimiza wenyewe wakiongozwa na waalimu, wakiwawezesha kwa kuwapa nyenzo na fursa kielimu. Usimamizi mzuri wa darasa unategemea utumiaji wa nyenzo zisizo za unyanyasaji katika kudhibiti tabia mbaya kwa watoto, pamoja na waalimu waliofunzwa vyema kuwaongoza wanafunzi katika mandhari ambayo yanatoa msaada kwa watu wazima na watoto.

Watoto hawaonwi kama wamilikiwa wa wazazi tena bali kama binadamu walio na haki zao, na mabadailiko haya ya kimaoni yanatumika sawa kwa waalimu na watu wengine wanaowatunza watoto kwa niaba ya wazazi Kibinadamu, watoto wanafurahia haki zao- na haki hizo haziishii katika malango ya shule. Watoto wana haki sawa na watu wazima za kujilinda dhidi ya unyanyasaji wa kuumizwa na kupigwa. Hata ikiwa adhabu itolewayo inathaminiwa na sheria za shule, Kumpiga mtoto kunakiuka maadili na haki zake za kuheshimu uadilifu wa kimwili. Na adhabu zote za viboko ambazo zinakubalika kisheria zinaonyesha ukiukaji wa haki za watoto za kulindwa kutokana na mashambulio.



Baadhi ya shule za kidini zinaeleza kwamba imani zao zinawalazimu kutumia adhabu ya viboko. Je, ni ubaguzi kuwazuia kuitumia?

Baadhi ya shule za kidini zinaeleza kwamba imani zao zinawalazimu kutumia adhabu ya viboko. Je, ni ubaguzi kuwazuia kuitumia?

Baadhi ya shule za kidini zinarejea nukuu za kidini kwamba zinalazimu kutumia adhabu ya viboko. Lakini kupiga watoto si hatua inayoendana na maadili, na imani za mashirika makubwa ya kidini, ambayo yanakiri huruma, usawa, haki na kukataza ukatili. Wafuasi wa dini za ulimwengu wanaiga maisha yao kwa mfano na mafundisho ya waanzilishi wao. Wasomi na wanathiolojia wanasisitiza kwamba hakuna ushahidi wowote uliorekodiwa wa waanzilishi wa dini kuu kuhusu kumpiga mtoto.

Mtazamo wa kidini ambao unaruhusu adhabu ya viboko kwa watoto mara nyingi unatokana na utamaduni kiimla, nguvu na udhibiti wa watoto. Unazingatia utiifu potofu kama wema na unyanyasaji wa kimwili kama jibu sahihi kwa watoto ambao hawana tabia njema.

Viongozi wa kidini ni baadhi ya waharakati wa kidunia wa kokumesha adhabu ya viboko kwa watoto. Zaidi ya viongozi 800 wa kidini waliunga mkono mkataba katika Mkutano wa Ulimwengu wa Dini wa Kuombea Amani mjini Tokyo, Japan (2006) Kongamano la Kidini la Kupigania

Kusitisha kwa Unyanyasaji wa Watoto (Makubaliano ya Kyoto)[10] ambalo linaomba serikali kutumia sheria ambazo zinakataza unyanyasaji wa aina yoyote kwa watoto, ikiwa pamoja na adhabu ya viboko.[11]

Kamati ya Haki za Watoto, katika Nukuu yake nambari 8 inasisitiza kwamba haki za kidini zina mipaka ambayo imewekwa ili kulinda haki na uhuru wa wananchi wengine.[12] Kamati inaeleza:[13]

"Baadhi ya sababu za kidini zilizotolewa kuhalalisha adhabu ya viboko, zikipendekeza kwamba ufasiri fulani kuhusu maandishi ya kidini zinatetea umuhimu wa kutumia adhabu hiyo. Uhuru wa kidini unahusisha watu wote kwenye Agano la Haki za Kiraia na Kisiasa (nakala ya 18) lakini maadili ya kidini yanapaswa yaendane na heshima kwa wote, hadhi ya binadamu na uadilifu wa kimwili..."

10. Maelezo yote kuhusu azimio hili yanapatikana kwenye churchesfornon-violence.org/wp/wp-content/uploads/2012/02/Violence-Against-Children-3.pdf.

11. For further information, see www.churchesfornon-violence.org.

12. Maoni ya Jumla Nambari 8, aya. 29.

13. Maoni ya Jumla Nambari 8, aya. 29.

Waalimu na wafanyakazi wengi wanapata shida kufundisha kwa sababu ya madarasa yaliyojaa kupita kiasi na ukosefu wa miundombinu. Je, si kutoa adhabu za viboko huongezea mifadhaiko yao?

Ubishi huu ni uafiki wa kweli ulio wazi: Kwa mara nyingi adhabu ya viboko inatolewa pale watu wazima wanapotaka kutoa hasira mioyoni mwao na sio kama kigezo cha kuwalea watoto. Shule nyingi zinahitaji miundombinu na misaada lakini hata kama matatizo ya watu wazima yatakuwepo, kuwanyanyasa watoto hakuwezi kukubalika. Utunzaji wa watoto haupaswi kutegemea kuboreka kwa hali za watu wazima, kama vile haki za wanawake zisivyoweza kusubiri hali za wanaume ziboreke.

Kwa vyovyote vile, kuwapiga watoto hakusaidii kuondoa mfadhaiko. Watu wakubwa ambao huwapiga watoto kwa hasira husikia hatia; wale wanaopiga bila ya kujali hisia hugundua kuwa wanakabiliana na watoto wenye uchungu na hasira. Maisha katika shule ambazo adhabu ya viboko imesitishwa ili kuruhusu kuwepo kwa njia chanya za kutia nidhamu hupunguza msongo wa mawazo kwa wahusika wote.

Ni kweli kwamba walimu wengi wanafanya kazi katika hali ngumu sana. Wanaweza kupatiwa mafunzo duni, kulipwa chini ya kiwango na kutothaminiwa, madarasa yao yanaweza kuwa makubwa, na shule zinaweza kukosa vifaa vya kutosha na utawala bora. Inaeleweka wanaweza kuwa wagumu kukubali mabadiliko katika mazoezi ya kufundisha ambayo hayaambatani na rasilimali au kuungwa mkono vya kutosha. Ili kuwasaidia walimu waweze kuachana na adhabu ya viboko serikali lazima ziwekeze katika mafunzo sahihi na kuwaunga mkono walimu, rasilimali za kutosha kwa shule na utawala bora wa elimu, na pia kutunga sheria kwa makatazo.

Pale inapoanzishwa vizuri, kwa mfano pamoja na mafunzo juu ya uthibitisho wa athari za adhabu ya viboko na faida za nidhamu bila vurugu, kuwafundisha walimu stadi mpya chanya za usimamizi wa darasa na kuondoa utumiaji wa adhabu ya viboko zinaweza kubadilisha taaluma ya ualimu na mazingira ya shule kwa manufaa ya walimu na wanafunzi vilevile.

Tayari tunayo sera ya shule/ wizara dhidi ya adhabu ya viboko. Je, kwa nini pia ni muhimu kubadilisha sheria?

Katika baadhi ya nchi, sera, maagizo/maelekezo na/au kanuni za nidhamu za kiwizara zinasema kwamba adhabu ya viboko haifai kutumiwa, lakini hakuna kizuizi katika sheria, ambayo aidha imekuwa kimywa juu ya swala hili au hudhoofisha sera kwa kuidhinisha wazi adhabu ya viboko.[14] Kukubali sera dhidi ya adhabu ya viboko ni kukiri kuwa adhabu hiyo siyo sawa na ni mbaya kwa kujifunza – lakini kushindwa kuunga mkono sera hiyo kwa sheria inatatanisha, inawaweka walimu katika msimamo wa kisheria usio wazi, na hailindi vya kutosha haki ya watoto ya kupata elimu salama, isiyo na vurugu.

Ni muhimu kuondoa adhabu ya viboko kwa kuwa na sheria inayoelezea wazi kuwa adhabu ya viboko haikubaliki tena.

14. Kwa orodha ya nchi ambazo zina sera dhidi ya adhabu ya viboko lakini hakuna makatazo katika sheria, angalia Mpango wa Kimataifa wa Kukomesha Adhabu Yote ya Viboko kwa ya Watoto (2015), Kutengeneza shule zisizo na ukatili: kuzuia adhabu zote za viboko. Ripoti ya Kimataifa 2015, uk 5.

Sehemu ya 3: Tovuti na rasilimali muhimu

Kamati ya Wataalamu wa Afrika juu ya Haki na Ustawi wa Mtoto (2011), Maelezo Kuhusu Ukatili dhidi ya Watoto
endcorporalpunishment.org/assets/pdfs/reference-documents/ACERWC-statement-on-VAC-2011-EN.pdf

Usimamizi wa Darasani Mtandaoni
classroommanagementonline.com/index.html

Kamati ya Haki za Mtoto (2001), Maoni ya Jumla Na. 1 juu ya "malengo ya elimu"
http://tbinternet.ohchr.org/_layouts/treatybodyexternal/Download.aspx?symbolno=CRC%2fGC%2f2001%2f1&Lang=en

Kamati ya Haki za Mtoto (2006), Maoni ya Jumla Na. 8 juu ya "Haki yakulindwa dhidi ya adhabu ya viboko na aina nyingine za adhabu za kikatili au za kudhalilisha (vifungu 19, 28(2) na 37, kwa pamoja)"
tbinternet.ohchr.org/_layouts/treatybodyexternal/Download.aspx?symbolno=CRC%2fC%2fGC%2f8&Lang=en

Kamati ya Haki za Mtoto (2011), Maoni ya Jumla No.13 juu ya "Haki za mtoto ya uhuru dhidi ya aina zote za dhuluma"
tbinternet.ohchr.org/_layouts/treatybodyexternal/Download.aspx?symbolno=CRC%2fC%2fGC%2f13&Lang=en

Baraza la Ulaya, kampeni za kikanda "Inua mkono wako dhidi ya kupigwa!"
www.coe.int/en/web/children/corporal-punishment

Baraza la Ulaya (2007), Kukomesha adhabu ya viboko ya watoto: Maswali na majibu, Strasbourg: Machapisho ya Baraza la Ulaya
rm.coe.int/CoERMPublicCommonSearchServices/DisplayDCTMContent?documentId=090000168046d05e

Ulimwengu wa Elimu
www.educationworld.com

Kampeni ya kimataifa ya elimu
www.campaignforeducation.org

Mpango wa Kimataifa wa Kukomesha Adhabu zote za Viboko kwa Watoto
www.endcorporalpunishment.org

Mpango wa Kimataifa wa Kukomesha Adhabu Yote ya Viboko kwa Watoto (2009), Kuzuia adhabu ya viboko kwa watoto: Mwongozo wa mageuzi ya kisheria na hatua nyingine
endcorporalpunishment.org/resources/resources-on-law-reform/legal-reform-handbook-2009

Mpango wa Kimataifa wa Kukomesha Adhabu zote za Viboko kwa Watoto (2012), Rasilimali kwa ajili ya kuondoa adhabu ya viboko shuleni
endcorporalpunishment.org/resources/thematic-reports/resources-for-eliminating-corporal-punishment-in-schools.html

Mpango wa Kimataifa wa Kukomesha Adhabu yote ya Viboko kwa Watoto (2015), Kuelekea shule zisizo na vurugu: Kuzuia adhabu yote ya Viboko. Ripoti ya Kimataifa 2015
endcorporalpunishment.org/resources/thematic-publications/schools-report-2015

Ushirikiano wa Kimataifa Kukomesha Ukatili Dhidi ya Watoto
www.end-violence.org

Mafunzo ya Gordon Kimataifa
www.gordontraining.com

Tume ya nchi za Amerika juu ya Haki za Binadamu (2009), Ripoti juu ya adhabu ya viboko na haki za binadamu za watoto na vijana
endcorporalpunishment.org/wp-content/uploads/key-docs/IACHR-report-on-corporal-punishment-2009.pdf

Jifunze Bila Kuogopa
plan-uk.org/act-for-girls/about-because-i-am-a-girl/learn-without-fear

Wazazi na Walimu Dhidi ya Ukatili katika Elimu
www.nospank.net/books.htm

Mpango wa Asia Kusini Kukomesha Vurugu Dhidi ya Watoto, kampeni ya kikanda "Ulinzi sawa kwa watoto"
www.saievac.org/cp

Agenda ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa 2030
www.un.org/sustainabledevelopment/

UNICEF (2001), Ulinzi wa Mtoto: nidhamu na dhuluma
www.unicef.org/teachers/protection/violence.htm

Ofisi ya Utafiti ya UNICEF – Innocenti (2015), Adhabu ya Viboko Shuleni: Ushahidi wa Muda Mrefu kutoka Ethiopia, India, Peru na Vietnam
www.younglives.org.uk/sites/www.younglives.org.uk/files/Corporal%20Punishment%20in%20Schools.pdf

Wakati wa kukomesha adhabu ya viboko kwa watoto umefika. Sasa watoto wana haki ya kuheshimiwa na kulindwa kutoka kwa aina zote za unyanyasaji!

Mpango wa Kukomesha Adhabu zote za Viboko kwa Watoto Duniani
(Global Initiative to End All Corporal Punishment of Children)

Mpango wa Kukomesha Adhabu zote za Viboko kwa Watoto Ulimwenguni unaendeleza uzuiaji na kukomesha adhabu za viboko na kutoa msaada wa kiufundi na ushauri wa bure kuhusu mageuzi ya vipengele vyote vya sheria.

www.endcorporalpunishment.org

info@endcorporalpunishment.org

www.twitter.com/Glendcorpun

www.facebook.com/Glendcorporalpunishment

Shirika la Save the Children Sweden

Shirika la Save the Children Sweden linaunga mkono kuzuiwa kwa adhabu za viboko katika mazingira yote. Mnamo mwaka 1979, shirika la Save the Children lilichangia kuifanya Sweden kuwa nchi ya kwanza ulimwenguni kupiga marufuku adhabu za viboko kwa uwazi. Shirika la Save the Children linashughulika kufanikisha marufuku ya kisheria na kukomeshwa kwa adhabu za viboko na kufanya suala hili kuwa ajenda ya kisiasa ulimwenguni kote.

info@rb.se

www.raddabarnen.se

resourcecentre.savethechildren.net

GLOBAL INITIATIVE TO
End All Corporal
Punishment of Children

Save the Children